# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
## CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

**015/2** **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 2**
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 2½** **8 Novemba 2001 mchana**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D
2. Jibu swali MOJA (1) kutoka kila sehemu.
3. Majibu yote yaandikwe katika insha.
4. Fuata kwa makini maelekezo ya kila swali.
5. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 2 zenye maandishi



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**Bismillahir – Rahmanir – Rahim**

## SEHEMU A (Alama 25)

### QURAN

1. Chambua kwa kina mafunzo ya Suratut – Tyn.

2. "Hakika sisi ndio tulioteremsha mawaidha haya, na hakika sisi ndio tutakaoyahifadhi". (15:9). Onesha utaratibu alioufuata Mtume (S.A.W.) katika kuihifadhi Q'uran katika msahafu.

3. Onesha udhaifu wa madai ya makafiri wa leo kuwa Muhammad (S.A.W.) ameitunga Quran kwa sababu za kisiasa.

## SEHEMU B (Alama 25)

### TAWHIID

4. Hakikisha kuwa katika Uislamu, suala la kumwamini Allah (S.W) si suala la kufuata mkumbo tu (kibubusa), bali ni la kisayansi.

5. "Yeye ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uongofu na dini ya haki ili aijaalie kushinda dini zote; ijapokuwa watachukia makafiri" (9.33). Pamoja na ahadi hii, eleza umuhimu wa Uislamu kuwa juu ya dini nyingine.

6. Nguzo ya kwanza ya Uislamu na ya kwanza ya imani zinashuhudia kuwepo kwa Allah (S.W.). Mambo gani yanayoshuhudia kuwepo kwa Allah (S.W.) katika dhati ya mwanadamu mwenyewe?

## SEHEMU C (Alama 25)

### TAREKH

7. "Mitume huzaliwa mitume". Chambua Mafunzo tunayopata kutokana na maandalizi ya ki-il-hamu yaliyompitia Mtume (S.A.W) kabla Mola wake hajampa utume rasmi.

8. "Wanataka kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao, na Mwenyezi Mungu atakamilisha nuru yake ijapokuwa makafiri watachukia". (61:8). Mambo gani yaliyopelekea kushindwa kwa vitimbi vya makafiri wa Kiqureysh katika kipindi cha makka cha utume wa mtume Muhammad (S.A.W)?

9. "Hawatakuwa radhi juu yako Mayahudi wala Manasara mpaka ufuate mila yao ------" (2:120). Bainisha chokochoko zao dhidi ya Dola ya Kiislamu wakati wa uongozi wa Mtume (S.A.W) na zinavyoendelezwa nchini mwako dhidi ya Waislamu.

## SEHEMU D (Alama 25)

### FIQH

10. Lengo la nguzo tano za Uislamu ni kuwaandaa Waislamu waweze kumwabudu Allah (S.W) katika maisha yao yote na kuwa makhalifa hapa ulimwenguni. Eleza ni kwa nini Waislamu hawafikii lengo hili.

11. Chambua maeneo yanayoonesha usawa baina ya wanaume na wanawake katika Uislamu.

12. Mwalimu Ambari alipofariki dunia aliacha binti wawili na kijana mmoja, mkewe na wazazi wake wawili kama warithi wake pekee. Mali pekee aliyowaachia ni shilingi 170,000. Alikuwa na deni la shilingi 20,000 na aliusia shilingi 30,000 zitolewe sadaka kwa ajili ya kujenga shule ya Kiislamu Mayomboni. Kwa kuzingatia sharia ya mirathi kama ilivyoainishwa katika Quran (4:11 – 12) gawanya urithi huu kwa kuzingatia wahusika.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org